Uwezo wa Taarifa katika Utawala wa Shule: Uzoefu wa HakiElimu

Japhet Makongo na Rakesh Rajani

HakiElimu: Mfululizo wa Mada za Uchambuzi Namba. 2003. 1S

Uwezo wa Taarifa katika Utawala wa Shule: Uzoefu wa HakiElimu[1]

Japhet Makongo na Rakesh Rajani[2]

1. Utangulizi

Utawala bora kwenye elimu unahusu kuwezesha viongozi wa shule na mtaa kuwajibika kwenye jamii za shule. Pia inahusu kuweka mazingira mazuri kwa wanajamii wakiwemo wazazi, wanafunzi na walimu ya kushiriki kikamilifu katika kuelewa na kuboresha maendeleo ya shule.Watu huwa wanajiamini zaidi na kuwa na shauku ya kushiriki katika maamuzi endapo wanashiriki kwenye kufikia maamuzi hayo, na kama wamepewa fursa ya kuuliza maswali kwa viongozi. Uongozi unaowajibika na maamuzi ya pamoja ndiyo nguzo mbili muhimu za utawala bora

Nguzo ya tatu ni upatikanaji wa taarifa. Maamuzi mazuri yanatokana na upatikanaji wa taarifa. Wanajamii na viongozi hawataweza kuongoza vyema wakiwa gizani. Taarifa zinahitajika kupima maamuzi yanayowahusu, kuchagua kati ya maamuzi mbalimbali na kukadiria ipasavyo.

Watu wanahitaji taarifa za aina mbalimbali, kama vile:

- taarifa kuhusu hali za shule zao
- taarifa kuhusu mambo mbalimbali ndani ya jamii zao
- taarifa kuhusu taratibu ya jinsi maamuzi yanavyofikiwa katika jamii; ikiwemo ya chaguzi na jinsi ya kuwaondoa viongozi madarakani
- taarifa kuhusu mambo ya msingi yanayogusa masuala ya sera na sheria yenye maslahi kwa maisha yao
- taarifa kuhusu jinsi watu wengine walivyopambana na changamoto zinazofanana na zao.

Uzoefu unaonyesha kuwa viongozi hufanya maamuzi kuhusu masuala ya shule bila ya kushirikisha au kuwajibika kwa wananchi. Upatikanaji wa taarifa, zikiwemo za sera na zinazohusu matumizi ya fedha, mara nyingi zimekuwa kwa wachache. Wanajamii, hususan fukara ama wenye pato dogo, mara nyingi hufanywa kuamini kuwa hawana haki ya kupata taarifa hizo au kuuliza maswali.

Serikali inaelewa mapungufu yote haya na mabadiliko yamo mbioni kugeuza utawala wa jamii kuwa wa kidemokrasia na uwajibikaji. Mageuzi ya Serikali za Mitaa yanasisitiza uwezo na rasilimali kufikia ngazi za wananchi. Kazi kubwa ya Serikali Kuu, kwa sasa, ni kuziwezesha halmashauri kutoa huduma, kuandaa na kuendesha sera, kufuatilia utendaji na kuhakikisha usambazaji na matumizi mazuri ya rasilimali. Kuziweka taarifa wazi na kuzisambaza kwa kila mtu ni jambo la muhimu katika kufanikisha hili. Kwa mfano Wizara ya Fedha sasa inachapisha taarifa za mgao wa kila kipindi ambao unapelekwa kwenye halmashauri kwa ajili ya sekta zilizopewa kipaumbele, ili wananchi waweze kufanya ufuatiliaji. Kwa upande wao, halmashauri za wilaya zinapaswa kutoa taarifa za mapato na matumizi za kila robo mwaka.

---

[1] Hii ina tofauti kidogo na mada illiyotayarishwa kwa ajili ya warsha "Kuendeleza Uwezo wa Kamati za shule" iliyoandaliwa na Mtandao wa Elimu Tanzania (TEN/MET) 2002. Mada hii ya Uchambuzi ilichapishwa kwa mara ya kwanza na HakiElimu katika lugha ya Kiingereza mwaka 2003

[2] Japhet Makongo ni Meneja wa Programu ya Utawala wa Jamii na Rakesh Rajani ni Mkurugenzi Mtendaji HakiElimu

Maendeleo katika sekta ya elimu pia yanadhihirisha mageuzi haya. Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi 2002-2006 (MMEM), unasisitiza juu ya kushirikisha jamii kupitia kamati za shule zilizochaguliwa kidemokrasia zenye majukumu ya kupanga, kutekeleza na kusimamia shughuli zote za maendeleo ya shule. Kwa maana hii kamati ya shule inatambulika kama nguzo muhimu kwa mageuzi ya elimu. Chini ya MMEM kiasi kikubwa cha fedha kinapelekwa moja kwa moja mashuleni kwa ajili ya ujenzi wa miundo mbinu na mambo mengine ya uboreshaji elimu.

Hata hivyo mafanikio ya haya yanahitaji uwezo mkubwa wa wahusika katika ngazi ya chini kujenga uongozi thabiti na wa uwajibikaji. Ni muhimu wapate taarifa sahihi, wawe na uwezo wa kuzichambua na kuzisambaza. Kujibu changamoto hii ni nia kubwa ya HakiElimu.

Ripoti hii imegawanyika sehemu nne. Ya kwanza ni Utangulizi. Sehemu ya pili inaelezea baadhi ya shughuli za programu ya Utawala wa Jamii wa HakiElimu. Sehemu ya tatu inaorodhesha changamoto zinazokabili upashanaji taarifa na mawasiliano katika ngazi ya jamii. Na mwisho ni hitimisho fupi.

2. HakiElimu Inafanya Nini?

Mkakati wa HakiElimu ni kutoa nafasi kwa wananchi kushiriki katika utawala wa elimu kuanzia ngazi ya jumuiya, umma hadi ile ya uandaaji sera. Kuhusu ngazi ya mwanzo HakiElimu inafanya shughuli zake katika wilaya za Serengeti na Ukerewe (wilaya nyingine itaongezwa 2003). Lengo lake kubwa ni kuwawezesha wanajamii kuelewa na kushawishi za maamuzi ya shule, kujenga uwezo wa kidemokrasia na kuimarisha uwajibikaji wa menejimenti za shule. HakiElimu inashirikiana na wanafunzi, walimu, wazazi, wajumbe wa kamati za shule, mamlaka za halmashauri na vyama vya kijamii kuwawezesha kuvitumia vyombo vya mamlaka kufanikisha maslahi yao. Programu hii ina mambo mengi yanayoingiliana, kati ya hayo manne ni:

2.1 Kufanya uchunguzi kupata maoni ya jumuiya

Shughuli ya mwanzo inayofanyika katika kila wilaya ni kufanya utafiti kupata mawazo ya jamii kuhusu hali ya elimu na utawala wake. Mara nyingi watu wa kawaida ndiyo wanaoguswa na sera pamoja na utekelezaji wake. Msisitizo uko katika kujifunza kutoka kwa watu walio pembezoni, hususan maskini, wanafunzi na walemavu. Washiriki hupewa fursa ya kuelezea mazingira waliyomo na kuchambua sababu za kuendelea kwa matatizo yao na nini kifanyike ili kuyatatua. Kwa vile utafiti wa wilaya mbili za mwanzo uliingiliana na kuanzishwa kwa MMEM maswala mengi yamelenga juu ya vipengele muhimu vya mpango huu kama ambavyo wanajamii wanavyoona. Kwa mfano, mzazi mmoja alisema kwa msisitizo:

> *"… laiti kama Serikali ingetaka ushauri wetu juu ya watoto wapi tuwaingize shuleni, tungechagua kwanza wenye miaka zaidi ya saba. Hawa wadogo unaowaona hapa (akionyesha kundi la watoto wa darasa la kwanza), bado ni wadogo kuweza kutembea kutoka tunapoishi hadi shuleni kila siku. Pia ni hatari kwa sababu wapo wanyama wakali porini. Tunalazimika kuwapeleka shule kila siku na kama hatuwezi hawaendi!"*
>
> *(Mzazi wa kijiji cha Kebanchabancha, Wilaya ya Serengeti)*

Mwalimu mmoja nae alionyesha masikitiko yake juu ya sera ya kuandikisha watoto waliozidi umri wa miaka saba, katika mpango wa elimu isiyo rasmi MEMKWA, kwa kusema:

> *"Tulielezwa kutowaandikisha watoto hawa (wanaozidi miaka minane) na kuwa maelekezo yataletwa kutoka Wizara ya Elimu. Mara kwa mara wazazi wanatuuliza ni*

lini watoto wao wataanza madarasa ya MEMKWA. Wameshaanza kuwa na wasiwasi kwa sababu tayari watoto wao wameanza biashara ndogo ndogo na uvuvi. Inanichanganya laiti ningekuwa na namna ya kuwaeleza."

(Mwalimu wa kike shule ya msingi Bulamba, Ukerewe)

Mawazo haya yanaonyesha wanajamii hawakushirikishwa kwenye mipango ya sera. Pia hakuna aliyefikiria athari za sera hizo na hazieleweki vyema katika ngazi za chini.

2.2 Kuwezesha Upatikanaji wa Taarifa na Nafasi ya Mawasiliano

HakiElimu huwezesha kusambazwa na kupeana taarifa katika ngazi ya jumuiya ili kuchochea uelewa na utendaji kazi. Maeneo yanayozingatiwa ni pamoja na:

- *Taarifa kuhusu sera na sheria.* Ingawa Serikali ndiyo yenye jukumu la kusambaza taarifa za sera na kupanga sheria nchi nzima, mara nyingi hushindwa kufanya hivyo katika wakati mwafaka. Hivyo basi, HakiElimu imetoa na kusambaza nakala za ziada za MMEM na vipengele vyake kwa wakuu wa wilaya na kata, kamati za shule na walimu wakuu. HakiElimu pia, husambaza taarifa nyingine kuhusu sera za elimu na zile zinazohusu mabadiliko mbalimbali yanayofanywa na Serikali kuhusiana na elimu. Pamoja na kusambaza machapisho rasmi, HakiElimu inachambua kwa lugha rahisi taarifa nyinginezo za elimu kwa umma zinazohusu vipengele muhimu vya sera na kuzisambaza kwa wanajamii. Kalenda ya mwaka 2002, iliyotolewa na HakiElimu, yenye ujumbe juu ya jambo moja muhimu la MMEM, ni mfano mmoja.

- *Maoni ya jamii juu ya elimu.* HakiElimu inafanikisha majadiliano mashuleni na vijijini kuwezesha wanajamii kujadili masuala yanayowagusa kuhusiana na elimu. Kwa kushirikiana na maofisa elimu wa wilaya na kata pamoja na kamati za shule HakiElimu, hivi karibuni, imeanzisha mijadala juu ya umuhimu wa sera za taifa katika maeneo ya watu. Baadhi ya mambo muhimu yaliyojitokeza ni pamoja na maswali kuhusu ubora wa utoaji elimu, umri wa kuandikishwa, vigezo vya kutumika kufuatilia matumizi ya ruzuku na jinsi ya kuboresha uwajibikaji kwenye masuala yanayohusu fedha. Mawazo ya msingi juu ya utendaji mzuri wa kutoa elimu bora mara nyingi hujitokeza katika vikao hivi. Wakati mwingine HakiElimu hushindanisha watu ili kupata mawazo ya wanajamii juu ya "Nini maana ya shule bora?" Matokeo hupelekwa kwenye vyombo husika kama vile Serikali za Mitaa, Wizara ya Elimu na Utamaduni na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

- *Vyombo vya habari vya Kijamii.* Upashanaji wa taarifa ni changamoto kubwa vijijini, ambako vyombo vya mawasiliano ni duni. HakiElimu inashawishi wanajamii kutumia teknolojia rahisi kama vile mbao za matangazo, michoro na mabango ambayo huwekwa sehemu za wazi mashuleni, sokoni na majengo ya Serikali kama njia ya mawasiliano. HakiElimu iko mbioni kuwapatia mafunzo waandishi wa habari vijijini pamoja na vifaa vya kuandikia, kamera na usafiri ili kufuatilia kero na mafanikio ya elimu kwa kutumia nyenzo hizi. Matumizi ya vikundi ndani ya jamii, kama vile W*agosi wa Kaya* na nyimbo ya *walimu* na *ndiyo mzee* ambayo huanzisha mijadala yanaendelezwa.

2.3 Kuendeleza ushirikiano na kujifunza

HakiElimu ina mpango wa kuendeleza mafunzo na ushirikiano na wilaya. Hii ni pamoja na kuwezesha mashule na jumuiya kujenga ushirikiano wa karibu kati ya wadau juu ya changamoto zinazowakabili, mafanikio, uzoefu na jinsi ya kushinda matatizo yanayojitokeza mara kwa mara.

Ubadilishanaji uzoefu utahusu viongozi wa Serikali pamoja na wajumbe wa kamati za shule, wazazi, walimu na wanafunzi. Mambo yanayofikiriwa ni pamoja na kutembelea jumuiya yenye kamati ya shule iliyo na mipango mizuri, au kwa mtu mwenye upeo kuzitembelea jumuiya kadhaa. Yote haya yanaweza kuongeza mawasiliano ya mara kwa mara na kujifunza baina ya jumuiya. Njia nyingine za kutembeleana na kushirikiana katika kujifunza miongoni mwa wadau mbalimbali zinaandaliwa.

2.4 Kuweka kumbukumbu na kusambaza mambo tuliyojifunza

Mara nyingi sera za taifa huwa na mguso katika ngazi ya jumuiya, lakini hutolewa bila taarifa za kutosha kuhusu hali halisi ilivyo katika ngazi za chini. Taarifa hutoka juu na kwenda chini na aghalabu wanajamii hawana nyenzo za kuwawezesha sauti zao kusikika na waandaaji wa sera. HakiElimu itafanya kazi ya kuziba pengo hili kwa njia mbili kubwa: kufanikisha uwezekano wa wananchi wa kawaida na taasisi za wananchi kuwa karibu na wanaotoa maamuzi kwa kuweka kumbukumbu na kusambaza mambo tuliyojifunza, kwa Serikali, vyama vya kijamii na wafadhili. Msisitizo mkubwa upo katika kupeleka taarifa kwenye Kamati ya Maendeleo ya Elimu ya Msingi (BEDC) na kwa wajumbe wa Mtandao wa Elimu Tanzania (TEN/MET).

Wawezeshaji wa HakiElimu wa jumuiya walioko wilayani pamoja na washiriki wa vyama vya kijamii watakuwa na jukumu katika kufanikisha haya. Watasaidia kuwatambua wanajamii wenye uchungu au dukuduku za kupeleka mbele ya viongozi. Pia watatunza kumbukumbu za mafunzo yaliyopatikana katika maeneo yao, na kwa msaada wa mwandishi mwenye utaalamu wa kisanii na kwa namna inayosomeka bayana watayaandika na kusambaza nchi nzima. Vyombo vya habari pia vitashirikishwa katika kusambaza taarifa.

3. Changamoto

Kuziwezesha jamii kupata taarifa muhimu pamoja na kuziwasilisha taarifa zao kwa mamlaka husika, ni jambo lenye changamoto. Baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na:

3.1 Gharama kubwa za mawasiliano. Gharama za uchapaji, mashine za kutolea vivuli na karatasi ni kubwa mno, na kwa baadhi ya maeneo hazipatikani kabisa. Kwa mfano Nansio, Ukerewe, gharama ya kutoa nakala kivuli ni shilingi. 200/= kwa karatasi moja! Huduma za simu ziko mijini tu, kwenye ofisi za Serikali na za wafanyabiashara.

3.2 Utunzaji mbovu wa kumbukumbu. Uzoefu mdogo na ukosefu wa vifaa unafanya utunzaji wa kumbukumbu kuwa wa kiwango cha chini katika ngazi ya vijiji. Baadhi ya kamati za shule hazitunzi dondoo na kumbukumbu za mambo yaliyojadiliwa. Mbao nyingi za matangazo ni kwa ajili ya mahudhurio ya wanafunzi na hamna chochote kwa ajili ya wanajamii kupata taarifa. Sehemu nyingine vitu vya msingi kama mbao za matangazo na makabati hamna kabisa. Tatizo lingine ni ukosefu wa waliokabidhiwa dhamana ya kutunza kumbukumbu kujihusisha na kumbukumbu hizo. Wanazitoa kwa wakubwa wao pasi na wao kuzitumia. Mambo haya yanachangia kuinyima jamii taarifa muhimu.

3.3 Taarifa kukosa mvuto. Mara nyingi wanajamii hawaoni umuhimu wa taarifa zinazotolewa na Serikali au vyama vya kijamii, kwa sababu lugha inayotumiwa katika vipeperushi na vijitabu vyenye maelekezo mafupi haina mvuto wowote. Taarifa zinakuwa kama mahubiri badala ya kushawishi.

3.4 Matatizo ya usambazaji. Taarifa chache zinazopatikana katika ngazi ya wilaya na kijiji huhodhiwa kwenye mafaili. Ni kawaida kukuta vipeperushi na ripoti zenye taarifa kuhusu utekelezaji zimerundikana maofisini, huku viongozi wakilalamikia ukosefu wa taarifa hizo.

Pia tatizo la usafiri na uangalizi mbovu wa taarifa kwa ajili ya jamii husababisha taarifa kubaki kwenye ofisi za wilaya badala ya kupelekwa vijijini. Kwa mfano vifaa vilivyosambazwa na Serikali pamoja na HakiElimu juu ya MMEM na vilivyotoka Ofisi ya Makamu wa Rais/Hakikazi kuhusu sera ya kuondoa umaskini, vimeonekana vikizagaa kwenye baadhi ya ofisi za wilaya. Hata pale ambapo vifaa vinasambazwa, hakuna maelekezo ya namna ya kuvitumia.

Mfano huu unadhihirisha:

> *"…tumepokea hizi (kabrasha za MMEM) kutoka kwa Ofisa Mtendaji wa kata, lakini hatuelewi tuzitumieje…"*
>
> *(Mwalimu wa Shule ya Msingi, Busagani*)

Tatizo lingine ni kuwa, vifaa vilivyopo mara nyingi havitumiki, moja ya sababu ni kuwepo kwa desturi ndogo ya kutaka kujua, kuelewa na kutafuta taarifa mpya miongoni mwa jamii.

3.5 *Jamii kutopewa nafasi kueleza mawazo yao*. Ipo nafasi ndogo sana ya watu wa kawaida kutoa mawazo yao na yakakubalika. Hata kwenye vikao rasmi kama vile vya mabaraza ya vijiji na kamati za shule, kinachofanyika ni kwa viongozi kutoa maagizo tu. Wananchi hawapewi mwanya wa kutoa hoja na tathmini zao. Hata mikutano ya hadhara, kama ya mabaraza ya vijiji au kamati za shule, mara nyingi yanatumika kwa viongozi kutoa maagizo na ushauri toka juu. Katika mikutano hiyo washiriki hupewa nafasi ndogo ya kutoa michanganuo yao na tathmini nyingine. Wawakilishi wengi katika taasisi hizo hawajali na hawawajibiki kwa wanaohusika. Akielezea malalamiko waliokuwa nayo, mzazi mmoja wa kijiji cha Busagani, Ujerewe, alisema:

> *"Wawakilishi wetu katika kamati za shule hawatuambii walichojadiliana katika mkutano. Tunaambiwa na kushurutishwa tuchange fedha au tushiriki kwenye ujenzi. Napenda kuchangia shule, lakini nataka maelezo kwa nini wameweka kiasi hicho na kutulazimisha kwa nguvu…"*
>
> *(Mzazi kijiji cha Busagami)*

3.6 Hofu ya uwazi na kuogopa kuumbuliwa. Ugumu wa kupata taarifa kutoka idara za Serikali unatokana na urasimu wa kufanya kila kitu si kwa matumizi ya umma. Sehemu nyingine viongozi walio juu hawako tayari kukosolewa. Mara nyingi majibu ni 'mimi sio msemaji wa idara'. Pia viongozi wengi hawajui namna ya kufanya kazi na vyama vya kijamii vinavyotetea maslahi ya wananchi.

4. Hitimisho

Kama ulivyo msemo wa zamani; taarifa ni nguvu. Wananchi katika ngazi ya jumuiya hawawezi kuboresha hali ya elimu kama hawapatiwi taarifa muhimu na nafasi ya kuzijadili. Watoa maamuzi hawawezi kutoa maamuzi au sera zenye mwelekeo kama hawapati taarifa, kukosolewa na kujifunza kutoka ngazi za chini.

Ndiyo maana taarifa ni muhimu kwa utawala wa kidemokrasia katika elimu na ndiyo sababu HakiElimu inatafuta kuwezesha upatikanaji wake na kurahisisha mawasiliano. Tunataka kuchochea na kuunga mkono vikundi vya kijamii kubadili hali za shule kuwa za kidemokrasia. Kwa kufanya kazi pamoja tunategemea kuonyesha kwamba, upatikanaji wa habari kuhusu elimu na kusambaa kwake ni muhimu kama ilivyo kujenga madarasa, mafunzo ya walimu, upatikanaji wa vitabu na mambo mengine yanayohusu elimu.

Inawezekana siku moja ikatokea kila mwanafunzi na kila mzazi atakuwa na uelewa juu ya bajeti ya shule ama kuweza kuuliza maswali. Ambapo kamati za shule zitakuwa vikao vya raia wa kawaida kujadili na kutatua matatizo. Pia maofisa elimu wa wilaya watachukulia majadiliano ya pande mbili pamoja na shule kuwa sehemu ya majukumu ya kazi zao. Pengine siku itafika ambapo viongozi wataona umuhimu wa kujadiliana na wananchi kabla ya kutoa maamuzi makubwa kuhusu masuala ya nchi, na kuwasikiliza watu hata kama taarifa walizokuwa nazo zinapingana na mitazamo yao. Hii itakuwa siku ambapo mwananchi wa Tanzania atakuwa na uwezo wa kubadili hali ya shule yake kutoa elimu bora.